Maswali yanayoulizwa mara kwa mara kuhusu chanjo ya COVID-19

#ThisIsMyWhy

Kwa nini nipewe chanjo ya COVID-19?

COVID-19 inaweza kusababisha ugonjwa mbaya au hata kifo. Hakuna njia ya kujua jinsi COVID-19 itakuathiri. Na ikiwa utaambukizwa virusi, unaweza kueneza kwa marafiki, familia na wengine walio karibu nawe, hata ikiwa huna dalili au ukiwa na dalili hafifu. Chanjo zote za COVID-19 zinazopatikana sasa nchini Marekani zimeonyeshwa kuwa nzuri sana katika kuzuia COVID-19. Hata ikiwa utaambukizwa baada ya kupata chanjo, chanjo inaweza kukuzuia usiwe mgonjwa sana.

Je, chanjo inaweza kuniambukiza COVID-19?

La, chanjo haisababishi COVID-19. Hakuna chanjo yoyote iliyoidhinishwa ya COVID-19 iliyo na virusi vinavyosababisha COVID-19. Inachukua wiki chache baada ya chanjo kwa mwili wako kuunda kingamwili za kukukinga na virusi. Hiyo inamaanisha kwamba inawezekana kuwa unaweza kuambukizwa virusi vinavyosababisha COVID-19 kabla tu au baada tu ya kupata chanjo na bado uwe mgonjwa.

Je, chanjo itaniumiza au itanifanya niwe mgonjwa?

Watu wengine wanaweza kupata misuli yenye vidonda, kuhisi uchovu au kuwa na homa hafifu baada ya kupata chanjo. Athari hizi zinamaanisha chanjo inafanya kazi ili kusaidia kufundisha mwili wako jinsi ya kupambana na COVID-19 ikiwa umewekwa katika hatari ya kuambukizwa. Kwa watu wengi, athari hizi hazitadumu zaidi ya siku chache. Ikiwa una wasiwasi wowote, piga simu kwa daktari wako au muuguzi.

Je, ninapaswa kupata chanjo ikiwa tayari nilikuwa na COVID-19?

Ndiyo, unapaswa bado kupewa chanjo kwa sababu unaweza kuambukizwa zaidi ya mara moja. Ingawa unaweza kuwa na kinga ya asili ya muda mfupi (inayojulikana kama kingamwilini) baada ya kupona kutokana na COVID-19, hatujui kinga hii itachukua muda gani. Chanjo ndio kinga bora, na ni salama. Watu wanaoambukizwa COVID-19 wanaweza kuwa na magonjwa mabaya, na wengine huwa na dalili zinazoendelea kwa miezi. Ikiwa umekuwa na COVID-19, muulize daktari wako, muuguzi au kliniki wakati unapaswa kupewa chanjo.

Ninaweza kupewa chanjo lini?

Idara ya Afya ya Umma ya Massachusetts imeweka ratiba ya chanjo hiyo, katika awamu tatu, kuanzia na wafanyakazi wa huduma ya afya na watu wazee/watu walio wagonjwa zaidi na kumalizia na umma kwa jumla. Nenda kwenye **www.mass.gov/covid-19-vaccine** ili kujua ni lini unaweza kupewa chanjo. Chanjo itakapopatikana kwa watu wa umma kwa ujumla, kliniki za chanjo za umma zitapatikana kwenye tovuti ya maingiliano ya CDC: **www.vaccinefinder.org**. Jimbo la Massachusetts pia lina maeneo ya chanjo yaliyofunguliwa. Ili ujisajili, unaweza kutembelea **mass.gov/COVIDVaccineMap**.

Greater Lowell Health Alliance: **greaterlowellhealthalliance.org/covid-19**
Lowell Community Health Center: **lchealth.org/patients/covid-19-updates**
CDC: **cdc.gov/coronavirus/2019-ncov/vaccines/faq.html**
MA DPH: **mass.gov/info-details/covid-19-updates-and-information#covid-19-vaccine-**

GLHA GREATER LOWELL HEALTH ALLIANCE

#ThisIsMyWhy

LOWELL COMMUNITY HEALTH CENTER

Mpango huu unategemezwa na fedha kutoka kwa Hazina ya Greater Lowell Community Foundation ya Kukabiliana na Dharura ya COVID-19

Je, itanilazimu nilipie chanjo?

La. Serikali ya shirikisho inatoa chanjo hiyo bila malipo kwa watu wote wanaoishi Marekani.

Je, ni chanjo gani iliyo bora?

Chanjo bora ni ile ambayo unaweza kupata. Chanjo moja sio bora kuliko nyingine. Chanjo zote ambazo zimeidhinishwa nchini Marekani ni salama na zinatoa kinga ili kuzuia ugonjwa mkali na kifo. Kamati ya Chakula na Dawa ya Marekani (FDA) iliidhinisha chanjo hizo kwa matumizi ya dharura, na madaktari na wataalamu wa kibinafsi walithibitisha kuwa chanjo hizo zinafikia viwango vya juu vya usalama.

Ni nani hapaswi kupewa chanjo ya COVID-19?

Kabla ya kupata chanjo, mwambie mtoa huduma wako wa chanjo ikiwa:

- Una historia ya athari kali za mzio
- Una homa ya joto
- Una shida ya kutokwa na damu au unatumia vipunguzi vya damu
- Una kinga dhaifu mwilini au unatumia dawa inayoathiri mfumo wako wa kingamwilini
- Una ujauzito, unapanga kuwa mjamzito au unanyonyesha
- Umepokea chanjo nyingine ya COVID-19.

Haupaswi kupata chanjo ikiwa umekuwa na athari mbaya ya mizio kutokana na dozi uliyopata awali ya COVID-19 au kutokana na kitu chochote kilicho kwenye chanjo hiyo. Chanjo hizo zina viungo zinazofanya kazi, messenger RNA (mRNA), pamoja na mafuta, chumvi, na sukari ili kulinda mRNA na kuisaidia kufanya kazi vizuri mwilini. Lazima uwe na umri wa angalau miaka 12 ili kupata chanjo, kulingana na chanjo unayopata.

Je, nitapata dozi ngapi na kutakuwa na muda gani kati ya dozi hizo?

Kulingana na chanjo ambayo utapokea, huenda ukapokea dozi moja au mbili, na dozi ya pili utapokea katika muda wa wiki tatu hadi nne baada ya kupokea ya kwanza.

Je, bado ninahitaji kuvaa barakoa na kukaa mbali na watu wengine baada ya kupata chanjo?

Watu ambao wamepata dozi kamili ya kujikinga dhidi ya COVID-19 wanaweza kukutana wakiwa vikundi vidogo bila kuvaa barakoa au kuweka umbali kati yao. Lakini kama uko pamoja na watu ambao hawajapata chanjo, bado unahitaji kuvaa barakoa, kukaa umbali wa futi sita kutoka kwao, na kunawa mikono mara nyingi.

*Kutoka kwa: CDC | Rev. 5/14/21



Kadi hii ya chanjo inapaswa kutumiwa kwa madhumuni ya kuonyeshana tu. **Usipatiane kamwe kadi yako iliyojazwa pamoja na habari zako za kibinafsi kwa watu wengine.**

Greater Lowell Health Alliance: **greaterlowellhealthalliance.org/covid-19**
Lowell Community Health Center: **lchealth.org/patients/covid-19-updates**
CDC: **cdc.gov/coronavirus/2019-ncov/vaccines/faq.html**
MA DPH: **mass.gov/info-details/covid-19-updates-and-information#covid-19-vaccine-**

GLHA GREATER LOWELL HEALTH ALLIANCE

#ThisIsMyWhy

LOWELL COMMUNITY HEALTH CENTER

Mpango huu unategemezwa na fedha kutoka kwa Hazina ya Greater Lowell Community Foundation ya Kukabiliana na Dharura ya COVID-19